

# MTIHANI WA KATI YA MUHULA WA PILI 2024

KIDATO CHA PILI

MAAKIZO

Maagizo

Fanya maswali vote

1) Sehemu ya A: USHAIRI (alama 15)

Ya mgambo imelia, masikio yategeni,

Inalo lahadithia, muhimu lenye thamani,

Muhimu kwetu insia, latufaa maishani,

Ufisadi tutengeni, unaturudisha nyuma

Papo hapo twakwamia, tuufanyapo mwandani,

Madawa kujiibia, huko hospitalini,

Kisha kwenda jiuzia, ndipo tupate mapeni,

Ufisadi tutengeni, unaturudisha nyuma

Kazini wakikujia, watu watoe dhikini,

Rushwa ukijidaia, bila ya haya usoni,

Ndiposa kuhudumia, sasa haya mambo gani?

Ufisadi tutengeni, unaturudisha nyuma

Faili kujichukulia, ukatia mvunguni,

Ndipo upate rupia, kuwadhili maskini,

Hwoni wajiharibia, kwa tamaa ya tumboni?

Ufisadi tutengeni, unaturudisha nyuma

Maswali

a) Je, hili ni shairi la aina gani? Toa sababu zako.( alama 2)

**Tarbia :kila ubeti una mishororo mine.**

- b) Toa kichwa mwafaka cha shairi hili.(alama 1)

**Ufisadi,ufisadi tutengeni.**

- c) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. (alama 4)

**Mshairi/nafsineni anasema kwamba mbiu ya mgambo imelia kwa hivyo watu watege masikio. Mbiu hii ina hadithi muhimu ya thamani ambayo sisi wanadamu inatuhusu maishani.kwa hivyo anasisitiza kwamba tuepuke ufisadi kwani unaturudisha nyuma.**

- d) Eleza muundo/umbo la shairi hili,( alama 5)

**Shairi hili beti nne.**

**Shairi hili lina mishororo mine katika kila ubeti.**

**Kila mishororo una mizani kumi na sita katika kila mishororo.**

**Shairi hili lina kibwagizo:ufisadi tutengeni,unaturudisha nyuma.**

**Vina vya kati na vya nje vinatiririka katika ubeti mmoja hadi mwingine.**

- 2.Eleza dhana ya istilahi hizi za kishairi.(alama 3)

- i. Mshororo mshata

**Ni mishororo ambao haujitoshelezi kimaana.**

- ii. Mshororo kifu

**Ni mishororo ambao ni kamili au unajitosheleza kimaana.**

- iii. Kibwagizo

**Ni mishororo wa mwisho katika ibeti unaorudiwa rudiwa.**

### **SEHEMU YA B: SARUFI (ALAMA 25)**

- a) Andika neno lenye muundo ufuatao.(alama 1)

Kitambaza,irabu ya chini kati,nazali ya ufizi,kipasuo ghuna cha ufizi,irabu ya chini kati

**Landa**

- b) Huku ukitoa mifano,eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili.(alama2)

**KKI-mtu**

**KKKI-mchwa**

**III-aua**

**KI-kitabu**

- c) Eleza maana ya shadda.(alama 1)

**Ni mkazo unaotiwa kwenye silabi au neno ili kuleta maana iliyokusudiwa.**

- d) Tunga sentensi kuonyesha majukumu yafuatayo.(alama 2)

i. Sentensi agizi **Niletee mayai mawili kwa soda.**

ii Sentensi hisishi **Lo! Hakingia kazini leo?**

- e) Fafanua maana ya mofimu huru.(alama 1)

**Hizi mofimu ambazo hujisimamia bila kuongezewa viambishi vyovyote.**

- f) Bainisha mofimu katika neno

Atamnywea

**a- Kiambishi cha nafsi/ngeli  
ta-wakati ujao  
m-yambwa/kitendwa/kitendewa  
nyw-mzizi  
e-kauli ya mnyambuliko  
a-kiishio.**

- g) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania.(alama 2)  
**Uchoyo wake ulimsababishia madhara mengi.**
- h) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi.(alama2)  
Mwanafunzi mkongwe amepewa tuzo kwa kuwa hodari masomoni.  
**Mkongwe-kivumishi cha sifa  
Hodari-kivumishi cha sifa**
- i) Tambua na ueleze aina za vitenzi katika sentensi hii. (alama 2)  
Mkulima angetaka kupalilia shamba lake mapema.  
**Angetaka-kitenzi kisaidizi  
Kupalilia-kitenzi kikuu  
Angetaka kupalilia-vitenzi sambamba**
- j) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vya pekee/halisi vyenye dhana zifuatazo:  
i) Bila kubakisha/kusaza **kivumishi -ote  
Vyote vimevunjika.**  
ii) Dhana ya umilikaji **kivumishi -enye  
Mwenye shamba amewasili.**  
iii) Bila kubagua/chagua **kivumishi-oote  
Chochote kizuri kimeliwa.**
- k) Unganisha sentensi zifuatazo kwa viunganishi mwafaka.(alama 2)  
Kheri aliweza kutujengea hospitali,Atajenga zahanati.  
**Kheri aliweza kutujengea hospitali halafu akajenga zahanati.**
- l) Ainisha vihusishi katika sentensi. (alama 2)  
Ame aliwasili mapema kuliko wengine halafu akaondoka.  
**Kuliko-kihusishi kilinganishi  
Halafu-kihusishi cha wakati**
- m) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi ya vielezi vifuatavyo.(alama 2)  
i) Kielezi cha namna kiigizi  
**Alianguka majini chumbwi.**  
ii) Kielezi cha namna kikariri  
**Alitembea haraka haraka.**

### **SEHEMU YA C: FASIHI SIMULIZI**

**“Kamba yangu ndefu lakini haiwezi kufunga kuni”**

- i) Tambua kijipera hiki. (alama 2)  
**Kitendawili.**

- ii) Eleza sifa nne za kijipera hiki.(alama 4)  
**Huwa ni semi fupi fupi zinazotumia lugha ya mkato.**  
**Hutolewa mbele ya hadhira ili vifumbuliwe.**  
**Hutumia lugha ya picha au taswira.**  
**Huwa na muundo/fomyula maalum.**  
**Hutegemea uwezo wa mtu kutambua na kuhusisha au kulinganisha vitu katika mazingira yake.**
- iii) Mwasilishaji wa kijipera hiki anafaa kuwa na sifa zipi?(alama 4)  
**Anapaswa kuwa na ubunifu wa kiwango cha juu.**  
**Mtambaji anapaswa kuijua hadhira yake.**  
**Anapaswa kuelewa mazingira ya hadhira yake.**  
**Anafaa kuwa mcheshi.**  
**Anafaa aishirikishe hadhira.**  
**Pia anafaa awe na ujasiri.**

